OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI RAU
S.L.P.1994
MOSHI

TAREHE …….

Simu; MKUU WA SHULE: 0754586720
Kumb. **Na RSS /JI / 11/ 144/K1 2021**
JINA LA MWANAFUNZI …….

P.O.BOX……MTAA / KIJIJI/ KATA ……

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA- 2021**

1. Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari Rau, iliyopo Manispaa ya Moshi, Kata ya Mfumuni Mtaa wa Ushirika barabara ya Uru karibu na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Umbali wa km $1\frac{1}{2}$ kutoka Makao Makuu ya Mkoa.
2. Kwa niaba ya Bodi ya Shule, Walimu na Wafanyakazi wasio – Walimu, tunakupongeza na kukukaribisha katika shule yetu. **Karibu sana**
3. Shule itafunguliwa Tarehe **…….** Ifikapo Tarehe **…….** kama Mwanao hajaripoti hapa Shuleni atakuwa amepoteza nafasi aliyopewa na **Taifa**.
4. Wanafunzi watakaotimiza maagizo yote ya kujiunga na Shule ndio tu watakaokubaliwa kuandikishwa na kuendelea na masomo. Matumaini ya Shule ni kwamba utatimiza kikamilifu maagizo ya kujiendeleza kielimu na kimaadili kwa faida ya Taifa kwa ujumla. Kama umekubali nafasi hii tekeleza maagizo yaliyoorodheshwa na jaza fomu A,B na C na kuzirudisha Shuleni Tarehe ya kuripoti.
5. Aidha kutakuwa na Mtihani wa kupima uwezo wa Wanafunzi utakaofanyika hapa Shuleni.
6. Masomo yanayofundishwa hapa Shuleni ni kama ifuatavyo:-
   Civics, History,Geography,Kiswahili,English, Biology, Chemistry, Physics, Mathematics, Commerce, Book keeping na Food and Nutrition (Chakula na Lishe) .
7. **MAJUKUMU YA MZAZI / MLEZI**:-
   Kufuatia agizo la Serikali la Elimu msingi bila malipo wazazi / walezi wana wajibu ufuatao;-

7.1 <u>SARE ZA SHULE:</u>

<u>WAVULANA:</u>

(i) Suruali mbili (2) **Kijivu - ISTEM / TAKRON** na 1, mashati mawili (2) meupe mikono mifupi,(**Tomato**) sweta **Kijivu** (2) **zinapatikana hapa Shuleni**.

(ii) Soksi nyeusi au kijivu jozi mbili (2)

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika mguu, vyenye kisigino kifupi viwe vya kamba au kuchomeka (gidamu na **SIO RABA.)**

N:B: (Surual iwe na marinda mawili na size kwa chini iwe 14cm na lazima iwe na turnup kwa chini)

WASICHANA:

(i) Sketi mbili (2) **Kijivu - ISTEM / TAKRON** na 1 , (**Rinda Box**) urefu inchi sita (6) toka unyayo / kiatu

(ii) Mashati mawili (2) meupe (mikono mifupi) (**Tomato**) **.**

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, vyenye kisigino kifupi,viwe vya kamba (gidamu), kuchomeka na **SIO RABA.**

(iv) Kwa wasichana wa madhehebu ya Kiislamu hijabu iwe nyeupe na ndefu wanaruhusiwa kuvaa suruali pia.

(a) Urembo wa aina yoyote hauruhusiwi kwa Wanafunzi (**mikufu, hereni, shanga, bangili**, **kupaka kucha rangi kufuga kucha n.k**) **Ni marufu kusuka nywele kwa wote.**

7.2 . **VIFAA VYA MAFUNZO**:

Kila Mwanafunzi alete vifaa vifuatavyo:-

(i) Madaftari makubwa kumi na mbili (12) kwa ajili ya darasani,(counter book Q 2)

(ii) Kamusi mbili ya Kiswahili na Kiingereza

(iii) Mathematical set, rula,penseli na kalamu ya wino

7.3. **KUWAPATIA WATOTO WAO CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA HUDUMA YA KWANZA**

KWA MAELEKEZO YA HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI SUALA LA CHAKULA CHA MCHANA CHA WANAFUNZI WOTE NI LAZIMA. NA KITACHANGIWA NA WAZAZI AU WALEZI KIASI CHA TSH. 97,000/= KWA MWAKA AU 48,500/= KWA MUHULA MMOJA. ACOUNT YA CHAKULA CHA WANAFUNZI RAU SEKONDARI NA: 40301100214 NMB AU WAKALA WA NMB POPOTE.

IELEWEKE WAZI KUWA HUDUMA YA CHAKULA CHA MCHANA NI LAZIMA KWA SHULE HII. HATUPOKEI KABISA MWANAFUNZI ASIYECHANGIWA CHAKULA .HILI LILIKUBALIWA NA WAZAZI NA BODI KURIDHIA KUWA ASIPOKELEWE KABISA MWANAFUNZI ASIYECHANGIA CHAKULA.

N:B FEDHA YOTE IWEKWE KWENYE A/C

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba **25 ya Mwaka 1978**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

NIDHAMU:

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuonyesha heshima Shuleni na anapokuwa nje ya Shule.

(ii) Kuheshimu na kuwatii Walimu na Wafanyakazi wasio Walimu.

(iii) Kuheshimu na kutii viranja na Viongozi wengine.

(iv) Kuheshimu Walimu / wageni wote wanaokuja Shuleni na kusaidia Wageni inapobidi.

(v) Mwanafunzi anatakiwa kupendana na wenzake na pia kuheshimiana.

(vi) Ni marufuku kupiga kelele Madarasani na kuongea kwa sauti kubwa ukiwa "**Smart area**" au nje ya **Darasa.**

(vii) Ni lazima kuzingatia **ratiba ya Shule**

(viii) Kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za Viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Shule.

(ix) Kuwahi Shuleni na kuondoka kwa muda uliopangwa.

(x) Usafi wa Mwili, Sare ya Shule na Mazingira ya Shule ni muhimu sana.

(xi) Mahusiano ya kimapenzi ukiwa Mwanafunzi ni marufuku, ukibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

7.4.**MAHUDHURIO:**

(i). Mwanafunzi anatakiwa kuwepo Shuleni muda wote wa saa za Masomo, ni marufuku kuzurura nje ya darasa muda wa vipindi.

(ii). Kuwahi Shuleni na kushiriki katika shughuli zote za Shule.

(iii). Mwanafunzi anatakiwa kuitikia maramoja na kukimbilia mahali husika asikiapo kengele au wito mwingine wowote.

(iv).Ni lazima Mwanafunzi awahi Shuleni Tarehe zilizopangwa mwanzoni mwa kila muhula, baada ya mapumziko ya aina yoyote.

7.5. **TAHADHARI:**

Ruhusa ya kutokuwa Shuleni siku moja au zaidi, ni lazima itoke kwa **Makamu Mkuu wa Shule** / Malezi / Mzazi / Mlezi aliyeandikishwa Shuleni ndiye atakayehusika kumwombea Mwanafunzi ruhusa na sio Mtu Mwingine yeyote.

7.6.**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(a) Wizi
(b) Uasherati, ushoga, ubakaji, kuwekwa unyumba.
(c) Ulevi wa aina yoyote, kama madawa ya kulevya, na pombe
(d) Kupiga au kupigana, pia kushiriki katika fujo au mgomo hapa Shuleni.
(e) Kuharibu kwa makusudi mali za Shule za Umma na kutoheshimu Bendera ya Taifa na picha za Viongozi wa Taifa.
(f) Kuoa au kuolewa akiwa shuleni.
(g) Kupata au kutoa mimba kwa wasichana na kuhusika na kutiamimba kwa wavulana.
(h) Kugoma,kuchochea mgomo, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa Shule / watu.
(i) .Kukataa adhabu au maelekezo ya Mkuu wa Shule / Mwalimu, Wafanyakazi wasio Walimu.
(j) Mwanafunzi kuwa na Simu ya mkononi, Redio ama vifaa vingine visivyo halali.
(k) Kupatikana na uhalifu au kumjeruhi mtu yeyote katika Jumuiya ya Shule hata nje ya Shule.
(l) Kucheza karata, kamari Shuleni.

16**. VIAMBATISHO:**

Form A,B, C na fomu ya mchanganuo wa malipo.

NB

i. Mzazi / Mlezi ahudhurie kikao kitakachofanyika Shuleni siku ya Jumamosi tarehe …… saa 3: 00 asubuhi bila kukosa.

ii. Hakikisha Mzazi / Mlezi unamleta Mwanao siku ya kusajiliwa Tarehe …….

KARIBUNI SANA RAU SEKONDARI

…….…….

AUGUSTINO L. SANGA
MKUU WA SHULE
03

FOMU 'A'

SHULE YA SEKONDARI RAU
S.L.P.1994
MOSHI.

MAKUBALIANO

KUKUBALI KUFUATA SHERIA ZA SHULE

Mimi _____nakubali nafasi ya kidato cha kwanza niliyopewa katika Shule hii.

Nayakubali **Masharti** na kuwa nitatii **Sheria** za Shule zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa Masomo yangu.

Naahidi kuwa nitaheshimu na kuwatii **Walimu** wote, **Watumishi wasio** Walimu kama walezi wangu.
Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa **Viongozi** wangu kwa mujibu wa **Sheria**.

Naahidi nitakuwa Mwanafunzi **Mwaminifu**, nitajielimisha kwa nguvu zangu akili zangu zote kwa manufaa yangu **binafsi** na **Taifa** langu. Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza **nafasi yangu** hapa Shuleni.

JINA LA MWANAFUNZI: _____

JINA LA MZAZI / MLEZI: _____

ANUANI YA MZAZI / MLEZI: _____

NAMBA YA SIMU YA MZAZI / MLEZI:_____

ANAKOISHI / MTAA / KIJIJI: _____

FOMU 'B'

SHULE YA SEKONDARI RAU
S.L.P. 1994
MOSHI.

MAELEZO BINAFSI

JAZA FOMU HII KWA USAHIHI NA KUIRUDISHA SHULENI SIKU YA KURIPOTI

1: Andika Majina Kamili:

JINA LA MWANAFUNZI	MAJINA MATATU	UMRI	TAREHE YA KUZALIWA
JINA LA BABA			
JINA LA MAMA			

2. Kijiji / Mtaa _____Kata ya_____
Tarafa_____Wilaya _____
Mkoa_____

4.Kukiwa na matatizo taarifa ipelekwe kwa **MZAZI / MLEZI**._____
Uhusiano_____anakofanya kazi _____
Mahali anapoishi _____namba ya **Simu _____**
Wazazi na Ndugu_____Baba yupo hai _____
Mama yupo hai_____Una Kaka wangapi? _____Una dada wangapi _____

5.Dini yako_____dhehebu_____

6. **Kama wewe ni Yatima;-**
(a) Unaishi na nani ? _____uhusiano:_____

(b) Nani anayekupa mahitaji ya Shule ? **JINA**: _____
MAHUSIANO:_____ **SAINI**_____

7.(a) Namba ya kitambulisho cha Taifa (**NIDA**) _____
(b)Kazi ya Mzazi / Mlezi _____
(c)Anuani ya Mzazi / Mlezi _____
(d)Namba ya Simu ya Mzazi / Mlezi _____

MEDICAL FORM

RAU SECONDARI SCHOOL
P.O.BOX 1994
MOSHI

To be completed by a **MEDICAL OFFICER** from a recognized Government **Hospital**

TO **MEDICAL OFFICER** ……

STUDENT'S FULL NAME:……**SEX / MALE**……

Blood count (Red and white) ……....

Stool Examinations……..

Sexually Transmitted: Diseases…….

T.B Test…….skin……..

Eye Test: ……Ears :……

Chest:…….Epleen :…….

Abdomen:…….....

ADDITIONAL INFORMATION

E.g. Physical defect / impairment, pediatric disorders : ……
I certify that the above is fit / unfit to pursue as stated above

Signature: ……..

Date : …….Official Rubber Stamp:

Note : The student should return the form dully completed to the school.